Habari mchanganyiko

Mhariri aliyeongoza sakata la Watergate afariki



WASHINGTON, MREKANI

BEN Brandlee, aliyekuwa Mhariri Mkuu aliyesimamia uchunguzi wa kashfa ya Watergate iliyomtoa madarakani Rais wa 37 wa marekani Richard Nixon, amefariki dunia Jumanne Wiki hii akiwa na umri wa miaka 93.

Brandlee, aliyekuwa mhariri wa gazeti la Washington Post, mwaka 1974 aliwatuma waandishi vijana wawili Bob Woodward na Carl Bernstein, kufuatilia kashfa hiyo iliyozua gumzo katika taifa hilo tajiri ulimwenguni.

Taarifa za kifo zake zilitolewa mapema Jumanne Wiki hii na kubainisha kuwa aliugua kwa muda mfupi na kufariki nyumbani kwake katika mji mkuu wa nchi hiyo Washington DC.

Donald E Graham, aliyekuwa mmiliki wa Washington Post wakati wa kashfa hiyo alimzungumzia Brandlee kama mhariri mahiri aliyewahi kufanya naye kazi.

"Ben Brandlee alikuwa mhariri mahiri wa magazeti katika taifa la Marekani alifanya mambo makubwa katika wakati wake hasa kuhusu uhariri wa kisasa," alisema Donald.

Ripoti ya gazeti hilo ilifunua uozo na mbinu chafu za serikali ya Marekani hata kusababisha Rais Nixon kutangaza kujiuzulu huku viongozi wengine wa serikali wakikumbana na mkono wa sheria.

"Ben alikuwa rafiki wa kweli, utaratibu wake ambao hakuubadili katika maisha yake yote ni kusema kweli na kushikilia njia za kuufuata ukweli, pia alikuwa na nidhamu ya jeshi," aliongeza Donald.

Rais Barack Obama, ambaye mwaka jana alimtunuku Brandlee nishani ya rais ya uhuru alisema mhariri huyo wa zamani ni mtu wa magazeti.

"Kwake uandishi wa habari ilikuwa zaidi ya taaluma, ni suala la kijamii hasa katika demokrasia yetu," alisema Obama.

"Katika kipindi cha uhariri wake kuanzia mwaka 1968 mpaka 1991, Brandlee aliwasaidia vijana kuandika habari na namna zinavyotakiwa kuandikwa, habari ambazo zilitusaidia kuielewa dunia kwa undani zaidi," aliongeza Obama.

Namna sakata la Watergate lilivyoripotiwa vizuri, lilisaidia kubadili mtazamo wa habari za uchunguzi nchini humo hata kusababisha kutungwa kitabu na baadaye kutengenezwa filamu iliyoitwa All the President's Men.

Katika mambo yaliyomuongezea umaarufu ni namna alivyoweza kutunza siri ya watoa habari wake, kwa sababu alikuwa miongoni mwa watu wachache waliomjua Mark Felt, ambaye ndiye aliyevujisha taarifa za sakata la Watergate, mpaka alipojitokeza hadharani mwaka 2005 na kujitaja kuwa yeye ni ofisa wa FBI.

LAPF: Deni la Serikali halijatuathiri

NA CLAUD GWANDU, Arusha

PAMOJA na kukiri kuidai Serikali karibu Sh bilioni 100, Mfuko wa pensheni wa LAPF umesema kuwa hali yake kifedha ni nzuri kuliko wakati

mwingine na thamani ya mfuko huo sasa imefikia sh. bilioni 700 huku ukikua kwa wastani wa asilimi 21 kwa mwaka.

Mfuko huo pamoja na mingine ya Hifadhi za Jamii, unaidai serikali zaidi ya sh. trilioni 7.5 ikiwa ni mikopo iliyotolewa kwa serikali katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vyuo vikuu, miundombinu ya barabara ba madaraja makubwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Pensheni wa LAPF, Eliud Sanga akiliri kwamba mfuko huo unaidai Serikali Sh bilioni 98 lakini deni hilo halina athari yoyote katika shughuli za maendeleo za mfuko huo.

"Ni kweli tunaidai Serikali sh bilioni 98 lakini tathmini ya mfuko inayofanywa kila baada ya miaka mitatu inaonyesha kwamba hali ya afya ya mfuko kifedha ni nzuri hivi sasa kuliko wakati mwingine wowote na ukuaji wa mfuko ni mzuri kuliko wastani wa asilimia saba uliowekwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii," alisema Sanga na kuongeza:

"Wanachama na wadau wetu hawana haja ya kuwa na wasiwasi na deni la serikali kwa kuwa kisheria Serikali ndio mdhamini mkuu wa mifuko yote ya hifadhi ya jamii,na sisi tunaendelea kutoa huduma bora ili kuwanufaisha wanachama wetu."

Alisema kuwa michango ya wanachama zaidi ya 127,000 na mapato yanayotokana na uwekezaji katika miradi mbalimbali ya kiuchumi yanauingizia mfuko huo zaidi ya sh bilioni 170 kila mwaka, na kwamba wamejidhatiti kuongeza wanachama zaidi katika setka isiyo rasmi.

Kuhusuu wekezaji, Mkurugenzi Mkuu huyo alisema kwamba Mfuko huo umejikita katika kutoa huduma bora zaidi kwa wanachama ikiwa ni pamoja na kuanzisha mfuko wa elimu ambao mwaka jana pekee umesaidia kuingiza wanachama 18,000 ambao ni walimu wa ngazi mbalimbali.

Meneja wa mfuko huo Kanda ya Kaskazini, Rajab Kinande alisema katika mkutano huo kuwa wanatarajia kuwekeza vitega uchumi vya majengo ya ofisi na maduka makubwa (Shopping Malls) baada ya kufanikiwa kupata viwanja katika maeneo ya Burka na Usa River,nje kidogo ya jiji la Arusha.

ACB yazindua huduma ya 'Golden Account'

NA DARLIN SAID

BENKI ya Akiba Commercial Bank (ACB) imezindua huduma mpya ya amana kwa wateja wenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea.

Akizungumza Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa ACB, John Lwande alisema lengo la kuanzisha huduma hiyo mpya inayofahamika kwa jina la ACB Golden Akaunti ni kuwarahisishia mteja wake kufikia malengo yao kupitia faida zitakazotokana na huduma hiyo. Pia kuhakikisha inatoa huduma bora za kifedha kwa kuzingatia kauli mbiu ya serikali ya kutoa huduma shiriki za kifedha (Financial Inclusion)

Lwande alisema mteja atakayetumia huduma hiyo ataweza kupata faida ya asilimia tatu ambayo itahesabiwa kila mwezi na kulipwa kila mwaka.

"Mbali na faida hiyo atapata bonus interest (faida ya ziada) kama atakuwa hajatoa fedha au ametoa mara moja katika kipindi cha robo mwaka pamoja na kupata mkopo hadi asilimia 80"alisema Lwande.

Aliongeza ili kuwafikia wateja wake benki hiyo iko mbioni kufungua tawi mkoani Mwanza ambapo kutaifanya kufikisha idadi ya matawi ya benki hiyo kufikia 17 .

Alisema tawi hilo litatoa huduma zote za kibenki kama kufungua amana, mikopo ya wajasiriamili wadogowadogo, wa kati na makampuni.

Gesi kutumika kuokoa misitu nchini

NA FELIX MWAKYEMBE

SERIKALI imeamua kutumia gesi asilia kuokoa misitu, lengo kuu ikiwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kupunguza matumizi ya nishati ya mkaa.

Katika kufanikisha mpango wake huo, hivi karibuni, serikali ya Tanzania ilizitaka nchi tajiri kusaidia katika mpango wake wa usambazaji gesi majumbani na viwandani ili kuachana na matumizi ya kuni, hatua itakayo okoa misitu hivyo kuchangia katika juhudi za dunia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Rais, Mazingira, Dk. Binilith Mahenge ameelekeza kidole chake kwa viongozi na maafisa wa serikali kwamba pamoja na vipato vyao kuwa vikubwa ikilinganishwa na wananchi wa kawaida na watumishi wa ngazi za chini, bado hutumia zaidi mkaa kuliko vyanzo vingine vya nishati.

Katika kukabiliana na kikwazo hicho, Waziri Mahenge amewachagiza wataalamu wa uchumi na masuala ya mazingira kufanya utafiti kwa watu wa matabaka yote ya kiuchumi, chini, kati na juu kubainisha sababu hasa zinazowasukuma kutumia mkaa kwa nishati.

"Ukiwauliza wengi watakueleza kuwa ni rahisi, ni vizuri sasa ifanyike study (utafiti) kwa watu wa hali ya chini, kati na juu, kufahamu sababu hasa za wao kutumia mkaa," alisema Dk. Mahenge akifungua Mkutano wa Nane wa Mpango wa Mazingira kwa Maendeleo Endelevu.

Kwa mujibu wa Waziri Mahenge zaidi ya tani 500 za mkaa hutumika nchini kwa mwaka, kiwango alichosema ni kikubwa ikilinganishwa kasi ya ustawi wa misitu nchini.

> **"Matumizi ya gesi asilia, hususani katika miji nchini, itasaidia kwa kiwango kikubwa utegemezi wa mkaa, ni kwa hatua hiyo itakayookoa misitu yetu**

"Matumizi ya gesi asilia, hususani katika miji nchini, itasaidia kwa kiwango kikubwa utegemezi wa mkaa, ni hatua itakayookoa misitu yetu," alisema Dk. Mahenge.

Mkutano huo umewakutanisha watafiti kutoka nchi mbali mbali duniani, zikiwemo Sweden , China, Chile, Kenya na wenyeji Tanzania, ambapo Mkurugenzi wa EFD, Prof. Gunnar Kohlin alibainisha kuwepo kwa pengo kati ya watafiti na watunga sera.

Maria van Berlekom alibainisha kuwa mwelekeo wa utajiri rasilimali unaogunduliwa nchini uwe kwenye umakini katika usimamizi wa utajiri huo wa rasilimali, ili hatimaye unufaishe taifa zima na watu wake.

Sweden imekuwa mfadhili muhimu wa kazi mbali mbali za kitafiti, na kutokana na umuhimu wa kazi hizo kwa maendeleo ya taifa, Maria alisisitiza nchi yake kuendelea kusaidia mipango ya kuwafikishia elimu, itokanayo na kazi za kitafiti, watunga sera pamoja na wananchi kwa ujumla.